**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**


# Karansi Secondary School
**P. O. Box 235, Sanya Juu,**
**Email:karansisecondary@Sihadc.go.tz**


Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KARANSI ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA MKOA KILIMANJARO MWAKA ………….**

**NAMBA ZA SIMU:**

**Mkuu wa Shule:** 0757504422

**Makamu Mkuu wa Shule:** 0764376482

**SHULE YA SEKONDARI KARANSI,**
S.L.P 235,
SANYAJUU-SIHA,
Tarehe …………………

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI………..............................……………………………….**

**S.L.P ……………………………………. ……………………………………………**.

Jumuia ya Shule ya Sekondari Karansi inayo furaha ya kukujulisha kuwa Mwanao ………………………………………….................................................................................. amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika mwaka wa masomo ………………. katika tahasusi ya **PCB/PCM** hongera sana. Shule ya Sekondari Karansi ipo Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro. Muhula wa masomo kwa kidato cha tano utaanza tarehe ………………. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe ……………. kuanzia **saa mbili asubuhi** hadi **saa kumi kamili jioni** na mahitaji yote yaliyoainishwa

Aidha mwanafunzi anatakiwa kuripoti ndani ya siku **kumi na nne** baada ya shule kufunguliwa.

## 1. MAHALI SHULE ILIPO

Basi unalosafiri nalo likifika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi mjini, Upande magari yanayoelekea stendi ya Sanya Juu kwa nauli ya shilingi Tsh. 4,000/=. Ukitokea Arusha Shukia stendi ya Bomang'ombe na kupanda gari la kuelekea Sanya Juu stendi kwa shilingi 2,000. Kisha usafiri wa kuelekea Karansi Senta ni shilingi 3,000/= kwa bajaji, Kutoka Karansi Senta hadi Shuleni ni Tsh. 4,000/= kwa usafiri wa Bajaji na Tsh. 2,000/= kwa usafiri wa pikipiki.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 2.1 SARE ZA SHULE

| S/N | AINA YA SARE |
|---|---|
| 1 | Sketi mbili (2) **draft kubwa rangi ya Dark green.** mshono **linda box** urefu ifike kwenye **kifundo** cha mguu. |
| 2 | Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu ya vifungo vya kawaida. |
| 3 | Hijab (Kijuba) rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia **iwe ndefu** kufikia kifundo cha mkono akisimama. |
| 4 | Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyokuwa na visigino virefu. |
| 5 | Soksi nyeupe ndefu pea tano |
| 6 | Tai mbili (02) rangi aina ya kitambaa cha sketi (sare ya darasani) |
| 7 | Sketi rangi ya bluu ya michezo fupi mshono linda za kawaida, T. shirt 2 moja nyeupe na nyingine rangi ya dark green zenye kola (form six) na raba nyeupe za michezo. |
| 8 | Gauni mbili za kushindia shuleni Zambarau nyeusi (Rangi dark puple) mshono wa solo lifike kwenye kwenye **kifundo** cha mguu (Na kwa watakao vaa Hijab iendane na rangi ya gauni la kushindia) |
| 9 | Track suit rangi kijani yenye mistari nyeupe pembeni (zisiwe za kubana). |
| 10 | Sweta rangi **DARK GREEN.** |
| 11 | Mto na Faronya ya rangi ya Blue Bahari, |
| 12 | Blanket zito kwa ajiri ya kipindi cha baridi |
| 13 | Chandarua, Shuka mbili Rangi Blue bahari |

| | |
|---|---|
| 14 | Khanga mbili au vitenge viwili. |

## 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI: -

| S/N | MAHITAJI |
|---|---|
| 1 | Godoro – Ukubwa wa futi “2$^1$/2” x” 6”. |
| 2 | Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe); |
| 3 | Ndoo mbili ndogo (za lita kumi) kwaajili ya kuogea na kuhifadhia maji ya kunywa. |
| 4 | Sanduku imara la chuma |
| 5 | Koti jeupe kwa ajiri ya maandalizi ya masomo ya vitendo (practicals) |
| 6 | Kwa wanafunzi wa tahasusi ya **PCB** waje na ‘disection kit’ pamoja na ‘disection tray’ ambavyo vitatumika katika masomo ya vitendo(Practicals) |
| 7 | Scientific Calculator (1) (fx 991 CASIO) |
| 8 | Stop watch (1), na graphs paper bando moja, Gloves bando moja kwa PCB na PCM, na mathematical set kwa PCM. |
| 9 | Mabuti **MAREFU** kwa ajili ya matope wakati wa mvua na maji. |
| 10 | Tochi ya solar |
| 11 | Passpoti size moja ya rangi. |
| 12 | Nakala(copy) ya cheti cha kuzaliwa |
| 13 | Nakala(copy) ya matokeo ya kidato cha nne (Result Slip) |
| 14 | Rimu 1 (A4) plain kwa muhula aina ya **PAPERLINE**. |
| 15 | Madaftari makubwa (Counter book quire 3) yasio pungua nane (8) |
| 16 | Nashauri Mwanafunzi anapo ripoti awe na Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu |
| 17 | Mwanafunzi aje na sabuni, taulo, kandambili, rangi (Kiwi) ya viatu vyeusi, mswaki, dawa ya meno, mafuta ya kupaka na nguo za ndani za kutosha. Mafuta ya kupaka aina ya **cream** na **marashi** haviruhusiwi**.** |
| 18 | **Vifaa vya usafi**: wanafunzi wa PCB walete moper( ndoo na dekio lake), sabuni ya maji lt 5, na fagio la kuondolea buibui na Chelewa, na wanafunzi wa PCM walete hardbroom, brash ndogo ya chooni, soft broom na squeezer na fagio la buibui. |

## 2.3 MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 01. | MCHANGO WA UENDESHAJI WA SHULE | 65,000/= |
| 02. | TAHADHARI | 5,000/= |
| 03. | NEMBO | 5,000/= |
| 04. | KITAMBULISHO CHA SHULE | 5.000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**NB:** Lipa Michango mbalimbali kwenye akaunti ya Shule No. **40101200097 NMB** JINA LA AKAUNTI: **KARANSI SECONDARY SCHOOL. Unapolipa kwenye Bank Pay in Slip iandikwe jina la Mwanafunzi**
Bank Pay in Slip iletwe Shuleni siku ya kuripoti ili ikatiwe risiti.

**VITABU VYA MASOMO KWA TAHASUSI (COMBINATIONS)**
Mzazi/mlezi anashauliwa kumnunulia mtoto wake vitabu vya masomo mbalimbali vinavyotumika kulingana na tahasusi aliyopangiwa.

| **SOMO** | **AINA YA KITABU** |
|---|---|
| Physics | Physics form V na VI vitabu vya TIE<br>ABC of physics,Fundamentals of physics,University physics volume I,Understanding mechanics,Engineering physics volume I,Principles of physics class xi and xii (S.Chand). |
| Advanced Mathematics | Pure Mathematics Kitabu cha TIE<br>Advanced level Maths(C.J.Tranter),Understanding mathematics,Mathematics xi(Chand Mathematics Volume 1 &2,Pure mathematics 1&2(Backhouse),Pure 1 and 2 (Bostock),The core mathematics,Engineering Mathematics, |
| Biology | Biology form V Kitabu cha TIE<br>Biology Form VI Kitabu cha TIE<br>Biological science (BS), Biological approach, Advanced<br>Biology (Nelson), Advanced Biology volume 1 &2 (S. Chand) |

| | |
|---|---|
| Chemistry | Genaral Chemistry Kitabu cha TIE<br>Physical Chemistry Kitabu cha TIE<br>Organic Chemistry Kitabu cha TIE<br>Inorganic Chemistry Kitabu cha TIE<br>Advanced level General and Physical Chemistry, Conceptual Chemistry volume 1&2, ABC Chemistry (S. Chand). |
| Basic Applied Mathematics | Basic Applied Mathematics Kitabu cha TIE. Ukikikosa unaweza nunua cha (S.Chand). |
| General Studies | Understanding advanced level General Studies (Johannes Bigirwamungu) |

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi **haruhusiwi** kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kuwa na nywele fupi wakati wote mwanafunzi awapo shuleni.
xiii. Mwanafunzi **haruhusiwi** kuweka nywele dawa wala kusuka.

xiv. Mwanafunzi **haruhusiwi** kuingia na chakula au kinywaji chochote shuleni

xv. Mwanafunzi **haruhusiwi** kuwepo bwenini wakati wa vipindi na muda wa **PREPARATION.**

xvi. Mwanafunzi **HARUHUSIWI** kwenda kwenye nyumba za watumishi bila ruhusa.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kufuga ndevu;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati na mahusiano ya kimapenzi;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za shule na nchi;

xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua; na

xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

**i.** Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

**ii.** Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

**iii.** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**iv.** Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KARANSI SEKONDARI

JINA LA MKUU WA SHULE: CATHERINE B. SHAO

SAINI YA MKUU WA SHULE:.........................

MHURI WA MKUU WA SHULE: ....................................

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0757504422**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0764376482**

**THE PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SIHA DISTRICT COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all form one and five students who join secondary school

## PART A
## TO THE MEDICAL OFFICER

**……………………………………………………………………………………………………………………**

**STUDENT FULL NAME ……………………………………………………………………………………….**

Please examine the above-named person as to be admitted to secondary school education

Signature ………………………………………. Designation……………………………………………

Name of head of school…………………………………………….

Official stamp ………………………………………….

## PART B: TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER

Blood count (white and red) ……………………………………………………………………………...

Stool examination ……………………………  TB Test ……………………………………………………. Eye test ……………………………………………  Ears test…………………………………………………………

Chest test………………………………………… Spleen test ……………………………………………………...

Abdomen test ………………………………… pregnancy (girls only) ……………………………………

## ADDITIONAL INFORMATION

Physical defect or impairment

………………………………………………………………………………………………………………. ………………

…………………………………………………………………………………………………………………….

Infection, chronic disease or family disease

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………

Other information

……………………………………………………………………………………………………………………. ..

Please certify that the above is fit to be enrolled at Karansi Secondary School

Signature …………………………… Designation ………………………………… station ……………………….

Date ………………………………

## PART C: MEDICAL OFFICER CERTIFICATION

I have examined the above person and consider that she/ he is/not fit physically to join to secondary school.

Medical officer's name ……………………………………………………. Signature ……………………………

Date ……………………………………………………………………

………………………………………………………………..

Official stamp

**HALMASHAURI YA WILAYA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI KARANSI**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi …………………………………………......mwenye umri wa miaka………… Jina kamili la baba……………………………………………………………………………….

Umri wa baba ni miaka………………Wilaya…………………… Tarafa………………..............

Kata…………………………… Namba ya simu ………………………...Dini…………………

Dhehebula…………...S.L. P………

Mimi mwanafunzi …………………………………………………… ninakiri kukubaliana na kufuata sheria zote za shule. Sahihi ya mwanafunzi ……………………………Tarehe…………

Mimi mzazi/mlezi wa ……………………………………………………. ninakubali/sikubali jukumu la ulipaji wa ada na michango ya shule.

Jina la mzazi/mlezi …………………………………………………Sahihi………………

Tarehe ………………………………………………

| Picha ya mzazi / mlezi |
|---|

| Picha ya mzazi / mlezi |
|---|

---

Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa au kuja kumtembelea mwanafunzi au kupewa taarifa za mwanafunzi endapo mzazi /mlezi hapatikani.

Jina kamili.........................................................................................................................................

Uhusiano wake na mwanafunzi ....................................................... namba ya simu................................